# MADHARA YA KUTAHIRI

# WANAWAKE

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# MADHARA YA KUTAHIRI WANAWAKE

# MADHARA YA KUTAHIRI WANAWAKE

**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**

**PREMIER PUBLISHERS CO LTD**
**DAR ES SALAAM**

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima,
S.L.P. 20679,
Dar es Salaam

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima,
Chapa ya kwanza 1992

Haki zote za kunakili zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kunakili au kukitoa kitabu hiki katika hali yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Kwa wale wote wenye nia njema ya kutokomeza mila ya kutahiri wana-wake

# WALIOSHIRIKI

Wafuatao walishiriki katika kukiandika kitabu hiki:

Dr.D. Kihwele - Muhimbili Medical Centre.

Dr.S.N. Massawe - Muhimbili Medical Centre.

Dr.M. Kaisi - Muhimbili Medical Centre.

Dr.G. Mduma - Wizara ya Afya

M.J. Rusimbi - CIDA

G.R. Mziray - UWT Makao Makuu

Dr.J.P.B. Mutangira- Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

M. Mponji - Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

L. Mahai - Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

A. Mrango - Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

E. Binagi - Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

B. Ngwawasya - Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

R.S Tembele - Mratibu wa Warsha, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

# DIBAJI

Kitabu hiki ni cha aina ya pekee kati ya vitabu vingi vilivyoandikwa na wanawake. Ili kukamilisha kazi ya uandishi wa kitabu hiki, semina, utafiti na taarifa mbalimbali zimetumika.

Haja kubwa ya kuandika kitabu hiki imetokana na madhara yaliyojitokeza bayana kutokana na kutahiri wanawake.
Mila na desturi za nchi yoyote lazima zitukuzwe na kuheshimiwa. Jinsi wakati unavyopita zipo aina za mila na desturi ambazo hazina faida kwa jamii, kinyume chake zinamdhalilisha mhusika.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa madhumuni ya kufafanua madhara yaliyojitokeza bayana kutokana na kutahiri wanawake.

Mbinu na mikakati imetolewa katika kutokomeza mila ya kutahiri wanawake. Hivyo wale wote ambao watabahatika kukipata kitabu hiki wakisome, ili lengo la ujumbe likamilike.

*E.N. Ntirukigwa*
*Mkurugenzi*
*Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima*
*Dar es Salaam.*

# SHUKURANI

Tunatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki katika kufanikisha utoaji wa kitabu hiki. Tukizingatia mila na desturi zinazotawala jamii nyingi hapa nchini, uandishi wa kitabu hiki juu ya somo hili nyeti la kutahiri wanawake, haukuwa rahisi hata kidogo. Iliwabidi waandishi wawe waangalifu sana na maneno ya kutumia na hapo hapo kuhakikisha kwamba ujumbe unawafikia walengwa bila ya kuwafanya waogope kukisoma kitabu. Waandishi wamefanya kazi nzuri sana kwa upande huu, hivyo wapokee shukurani za pekee.

Haitakuwa busara kuwasahau wafadhili wetu wa NORAD ambao wameonyesha ushirikiano mzuri sana na kutupa moyo wa kuendelea na suala hili tokea mwanzo wakati wanawake wa Wilaya ya Rombo walipolalamika gazetini kuhusu mila hii ya kutahiri wanawake. Shirika hili limetoa msaada wa kuendeshea warsha, utafiti na utoaji wa kitabu chenyewe.

Shukrani za pekee zimwendee pia Dr. J.P. B. Mutangira ambaye chini ya uenyekiti wake wakati wa warsha, kitabu hiki kiliweza kuandikwa kwa muda uliopangwa. Kadhalika Dr. Mutangira kwa niaba ya watafiti alieleza matokeo ya utafiti uliofanyika juu ya madhara ya kutahiri wanawake. Taarifa hii ilikuwa muhimu sana wakati wa kuandika kitabu hiki. Wote waliokuwa tayari kujibu maswali yetu wakati wa utafiti wanastahili shukurani zetu pia.

Hatuna budi pia kuwashukuru Ndugu A. Muze wa Dar es Salaam University Press na E.A. Mwasada wa TEWW kwa muda wao mwingi walioutumia katika kuhariri mswada wa kitabu hiki. Bila ya kazi yao nzuri, kitabu hiki kisingekuwa katika hali hii.

Mwisho tunapenda kuwashukuru wote waliofanikisha kazi hii ya kutoa kitabu hiki ambacho tunategemea kuwa kitatoa changamoto katika kutokomeza mila hii mbaya inayodhahilisha utu wa mwanamke

**Seksheni ya Elimu na Maendeleo ya Wanawake**

# YALIYOMO

Dibaji ........ vii

Shukrani ........ viii

Utangulizi ........ x

**SURA YA KWANZA:**
Utamaduni wa kutahiri Wanawake ........ 1

**SURA YA PILI**

Aina Mbalimbali za Kutahiri Wanawake ........ 7

**SURA YA TATU**

Madhara ya kutahiri Wanawake ........ 11

**SURA YA NNE**

Mbinu na Mikakati ya Kukabili na Kutokomeza Mila ya Kutahiri Wanawake ........ 15

# UTANGULIZI

Lengo kuu la kitabu hiki ni kuelimisha jamii juu ya utamaduni wa kutahiri wanawake na madhara yatokanayo na utamaduni huo. Hali kadhalika, nia nyingine ya kitabu ni kupendekeza mbinu na mikakati mbalimbali ambayo inaweza ikatumika katika kupambana na mila hiyo. Ili kufikia lengo hilo kitabu hiki kimegawanywa katika sura nne. Sura ya kwanza inazungumzia chimbuko la utamaduni wa kutahiri wanawake na maeneo ambayo yameathiriwa zaidi na utamaduni huo. Vilevile sababu mbalimbali zinazodaiwa kuwa ndiyo msingi wa utamaduni wa kutahiri wanawake zimejadiliwa. Sura ya pili inaelezea waziwazi aina mbalimbali za kutahiri wanawake. Sura ya tatu inaonyesha na kufafanua kwa undani zaidi madhara yanayotokana na kutahiri wanawake. Mathalani, madhara ya kisaikokojia, Kijinsia na kiafya.

Sura ya mwisho inajadili mbinu na mikakati mbalimbali ya kukabili na kutokomeza mila ya kutahiri wanawake; kama vile kuelimisha jamii kwa kutumia vyombo vya habari, semina, warsha, kongamano, mabango, majarida na vitini. Mbinu na mikakati hii itajumuisha Chama na Jumuiya zake, sekta mbalimbali za Serikali, madhehebu ya dini na mashirika ya watu binafsi.

Ni mategemeo yetu kwamba kitabu hiki kitatoa changamoto na mijadala itakayoambatana na vitendo halisi vya kupinga na hatimaye kutokomeza utamaduni wa kutahiri wanawake nchini Tanzania.

# Sura ya Kwanza

# UTAMADUNI WA KUTAHIRI WANAWAKE

Utamaduni, mila na desturi za nchi, mataifa na makabila mbalimbali vina mchango mkubwa katika uhai na maendeleo ya jamii. Hata hivyo, utafiti wa kisayansi umethibitisha kwamba, kuna baadhi ya utamaduni, mila na desturi ambazo kwa namna moja au nyingine, zinawadhalilisha na kuwakandamiza wanawake kijinsia. Dosari hii katika baadhi ya mila na desturi zinazotawala jamii zetu, hasa utamaduni wa kutahiri wanawake, ndilo chimbuko kuu la kitabu hiki.

Lazima izingatiwe kwamba wanawake ni sehemu kubwa ya watu na ni wazalishaji na walezi wakubwa katika nchi. Hivyo basi kuathirika kwao kutahatarisha kwa kiasi kikubwa maendeleo ya taifa zima.

Sura hii inajumuisha mchango wa mawazo ya wataalam wa fani za elimu ya jamii, saikolojia, saikolojia ya jamii, afya, utabibu, utafiti wa kitabibu na kijamii, na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Madhumuni ya sura hii ni kubadilishana mawazo juu ya chanzo na sababu zinazoambatana na utamaduni wa kutahiri wanawake. Aidha, matarajio ya mjadala huu ni kutafakari na kupanua mawazo yetu juu ya dhana, uhalali na athari zinazoambatana na utamaduni huu.

Chanzo cha utamaduni wa kutahiri wanawake:

Wataalam na Wachunguzi wengi katika suala zima la tohara ya wanawake wanadai kwamba kuna utatanishi juu ya chanzo halisi cha utamaduni huu. Hata hivyo, inakadiriwa kuwa utamaduni huu ulianza mnamo miaka 2000 iliyopita. 1. Utamaduni huu wa kutahiri wanawake umeenea sana Bara la

Asia na Afrika. Mathalan, utafiti uliokwisha fanyika unaonyesha kwamba zaidi ya wanawake 84 milioni katika Bara la Afrika wametahiriwa.

Baadhi ya maeneo ambayo yanatahiri wanawake ni: Mwambao wa Bahari ya Atlantiki, mwambao wa Bahari Nyekundu, Ghuba ya Uarabuni, Malaysia, Indonesia, na Australia (Waborijini). Maeneo mengine ni Nigeria, Bukina Faso, Mali, Senegal, Misri, Uhabeshi, Sudani, Somalia, Kaskazini mwa Kenya na Tanzania.

Hapa Tanzania, utamaduni wa kutahiri wanawake umeenea hasa katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara. Mathalan, mkoani Arusha, kuna ushahidi kwamba Wamasai, Wairaq na Wabarbaig hutahiri wanawake. Mkoani Dodoma pia, Wagogo na Wasandawi wana utamaduni huo huo. Wachaga na Wapare, mkoani Kilimanjaro, nao hutahiri wanawake. Wamwera, Wayao na Wamakua katika mikoa ya Lindi na Mtwara wana utamaduni huu vile vile. Hali kadhalika Wakurya, Wazanaki, Waikizu, Wasimbiti na Wasizaki mkoani Mara na Wanyaturu wa Singida wana utamaduni huo.

Kuna nadharia nyingi zinazohitilafiana kuhusu chanzo cha utamaduni huu wa kutahiri wanawake. Kwa hiyo ni vigumu kuthibitisha kama kuna chanzo kimoja au vyanzo vingi.

Ushahidi uliopo, unadhihirisha kuwa aina ya kutahiri wanawake ambayo imeenea Misri, Somalia na sehemu za Uarabuni chimbuko lake linatokana na utamaduni wa Misri ya kale. Baadhi ya makabila yanayoshiriki utamaduni huu wa kutahiri wanawake yanadai kwamba utamaduni huu ulikuwa ni sehemu muhimu ya tambiko la kiasili Barani Afrika, hasa kabla ya kuenea dini ya Kiislamu nchini Misri, Sudan na mwambao wa Bahari Nyekundu.

Jambo la kushangaza kuhusu utamaduni huo ni majina yanayotumika kuhusu kutahiri wanawake. Wasudani, mathalan, huiita 'tohara ya kifarao', wakimaanisha kwamba ina asili ya Misri. Hali Wamisri nao huiita 'tohara ya Kisudani'. Kila mmoja anadai ni utamaduni wenye asili katika nchi ya mwenzake. Ni dhahiri basi, kwamba tangu mwanzo utamaduni huu ulikuwa una walakini kiasi cha kuzifanya nchi zenye utamaduni huo kutouchukulia kama sehemu ya asili

yao. Aidha, Somalia kuitwa 'Ncni ya Wanawake Walioshonwa' inadhihirisha kwamba utamaduni wa kutahiri wanawake una asili ya namna fulani ya karaha yenye lengo la kumkandamiza na kumdhalilisha mwanamke.

Wachunguzi wa suala hili la kutahiri wanawake, bado hawajawa na uhakika ni kwa nini utamaduni huo unakua na kuimarika katika baadhi ya jamii; au haukukua na umetoweka katika jamii nyinginezo. Kimsingi ni kwamba, utamaduni huo bado upo, kwa hiyo ni lazima utokomezwe.

Sehemu inayofuata, tutaainisha kuchambua baadhi ya sababu ambazo inadaiwa zinaimarisha utamaduni wa kutahiri wanawake. Hii itatupatia mwanga zaidi juu ya utamaduni huu.

## Sababu za Kutahiri Wanawake

Uchunguzi unaonyesha kwamba, sababu zinazotolewa kuhusu umuhimu na umaarufu wa kutahiri wanawake zinahitilafiana kati ya nchi na nchi, hali kadhalika kati ya makabila mbalimbali katika nchi moja. Watafiti katika mambo ya jamii wamezigawa sababu zinazotolewa katika nyanja kuu nne sababu za kisaikolojia na kijinsia (psychosexual); sababu za kijamii, sababu zinazohusu hisia za kiafya na sababu za kidini au kiimani. Hebu tuzichambue sababu hizo kikamilifu.

### *1. Sababu za Kisaikolojia na kijinsia.*

Kuna sababu sita ambazo zimetolewa kuhusiana na uwanja huu katika tohara ya wanawake. Kwanza; baadhi ya jamii wanaamini kwamba kisimi kinawakilisha ujogoo au nguvu za kiume kwa vile kinaning'inia, na ni tishio kwa sehemu za siri za kiume. Hivyo, lazima kukata sehemu hiyo inayoning'inia.

Pili, kwamba sehemu hiyo isipokatwa, itasababisha ugumba (utasa) kwa mwanamke.

Tatu ni kwamba, kwa vile sehemu hiyo ya siri huning'inia, inaweza kuhatarisha uhai wa mtoto hasa wakati wa kuzaliwa.

Nne, imani potofu, hasa katika kabila la Wababambara nchini Mali kwamba binadamu anazo jinsia zote mbili, uume na

uke. Kisimi ni dalili ya uume kwa mwanamke na govi ni dalili ya uke kwa mwanaume. Hivyo ili kutofautisha kati ya mwanamke, lazima sehemu hizo zinazotatanisha zikatwe. Imani hiyo potofu pia inadai kwamba kisimi ni sumu inayoweza kumdhuru mwanaume wakati wa kufanya mapenzi.

Tano, kumtahiri mwanamke kunampunguzia ashiki au nyege. Hivyo kunalinda ubikira na kuzuia kutembea ovyo mitaani, hasa kabla na baada ya ndoa. Mara nyingi hoja hii si sahihi kwa sababu kisimi siyo sehemu pekee inayomfanya mwanamke apate ashiki. Hali kadhalika kukata kisimi hakulindi wala kutunza ubikira.

Sita, njia nyembamba inayobakizwa baada ya kumtahiri mwanamke ni mahususi kwa kuongezea starehe na burudani ya mwanamke wakati wa kufanya mapenzi. Aidha, kwa wanaume wenye wake wengi, tohara hii inampunguzia mwanaume lawama za kutojamii kwa vile mara nyingi wanawake wanakuwa hawana mshawasha wa kufanya mapenzi. Hivyo basi, kwa namna moja au nyingine, kutahiri wanawake ni njia ya kudhibiti jinsia zao. Inaelekea hata Tanzania sehemu ambazo wanatahiri wanawake, kudhibiti jinsia ya wanawake ndiyo sababu kuu inayotolewa. Mathalani, uchunguzi uliofanyika katika mikoa minne ya Tanzania bara (1989), umeonyesha kwamba wanawake wanatahiriwa ili kudhibiti mienendo yao kijinsia au kupunguza uwezekano wa uasherati. Jibu hilo lilitolewa na wahojiwa 176 kati ya 423. Sababu na imani zilizotajwa hapo juu hazina msingi wowote na ni potofu kabisa.

2.Sababu za Kijamii.

Kuna sababu kuu mbili kuhusu umuhimu wa kutahiri wanawake ambazo zimetolewa katika uwanja huu. Kwanza, kwamba ni mojawapo ya taratibu za unyago wa kuingia katika rika la utu uzima. Hoja hii imetetewa sana hata na baadhi ya viongozi wa siasa; mathalan hayati mzee Jomo Kenyatta katika kitabu chake mashuhuri Naushangilia Mlima Kenya. Kenyatta anadai kwamba mila hii ni muhimu katika kumuandaa msichana kuingia utu uzima hivyo ni lazima

ilindwe na kuimarishwa.

Pili, ni kwamba tohara ya wanawake huambatana na mafunzo maalum ya unyumba na wajibu wa mwanamke katika jamii. Hivyo basi, kutahiri kunazingatiwa kama sehemu muhimu jinsi yalivyo mafunzo hayo katika mfumo mzima wa utamaduni huu.

Hata hivyo, hoja ya kwamba, kutahiri wanawake kunawaandaa kuingia katika rika la utu uzima si sahihi. Mathalan, katika jamii nyingi imedhihirika kwamba wanawake hutahiriwa wakiwa na umri mdogo sana. Umri huo unaweza kuwa kati ya miaka miwili hadi kumi, ambao kisheria na kimaumbile siyo umri wa mtu mzima. Pia kama ilivyodhihirika katika jamii nyingi zisizotahiri wanawake, mafunzo ya unyago yanaweza kutolewa kwa msichana bila kufanya uharibifu katika viungo vya siri.

### *3. Sababu za Kiafya na Uzuri wa Kimaumbile Kihisia.*

Uchunguzi umedhihirisha pia kwamba kuna sababu mbili zinazotolewa kama msingi wa kuendeleza tohara ya wanawake katika uwanja huu. Kwanza, kiafya kisimi ni uchafu, mathalan, machoni mwa Wamisri na Wasudani. Sababu hii imejengwa katika misingi potofu.

Kinyume cha madai hayo hapo juu, ni kwamba uchunguzi wa kisayansi uliofanyika barani Afrika na sehemu zingine umedhihirisha kwamba tohara hizo zinasababisha mkusanyiko na mchanganyiko wa mkojo na hedhi. Hali hiyo huleta maumivu makali sana, kunuka, hali kadhalika uambukizo wa sehemu za siri za mwanamke.

Sababu nyingine ni ile inayoambatana na uzuri wa kihisia wa umbile la sehemu za siri za mwanamke. Jamii za Wamisri, Wasudani na Wasomali wanadhani, kwamba sehemu hizo za siri zinapaswa ziwe laini, nyororo na zilizosawazika ili kupendeza macho na hisia za mwanaume. Imani hii pia imeenea katika baadhi ya makabila nchini Tanzania. Sababu hii si kweli. Kwa mfano, utafiti uliofanyika (1989) unaonyesha kwamba wahojiwa wengi walidhihirisha kuwa wanavutiwa kufanya mapenzi na wanawake wenye viungo vyao kamili, na kwamba kutahiri wanawake ni kuharibu maumbile yao ya asili.

## 4. Sababu ya Kidini na Kiimani.

Sababu nyingine ambazo zinatolewa kama utetezi wa mila ya kutahiri wanawake ni maadili ya kidini, hasa dini za kiasili na dini ya Kiislamu. Kwa mfano huko Misri, Somalia na Sudani, na hata nchini Tanzania kama utafiti ulivyoonyesha, kuna baadhi ya watu waliojenga imani potofu kwamba dini ya Kiislamu inaagiza kwamba wanawake watahiriwe kama ilivyo kwa wanaume.

Wataalam na viongozi wa dini ya Kiislamu wanakataa kata kata kwamba hakuna msingi wowote wa kidini unaotukuza tohara ya wanawake. Hata hivyo, ni ajabu kwamba utamaduni huu bado unaendelea katika sehemu nyingi kwa visingizio vya kidini.

Tukirejea hoja zote zilizotolewa kwenye nyanja zote nne, ni dhahiri kwamba msingi wa utamaduni wa kutahiri wanawake unaambatana na imani potofu na mila na desturi, zenye lengo la kuwafurahisha wanaume hali utamaduni huo unaathiri afya na utu wa wanawake.

Utamaduni huu wa kutahiri wanawake umeanza kupigwa vita katika sehemu nyingi ulimwenguni. Nchini Sudani kuna kamati ya taifa inayoshughulikia mila na desturi zinazoathiri afya za wanawake na watoto, kutahiri wanawake ikiwa mojawapo ya mila hizo. Nchini Somalia kuna kampeni dhidi ya tohara kwa wanawake. Juhudi hizo pia zinafanyika nchini Mali, Bukina Faso, Nigeria na Uhabeshi. Nchini Tanzania kumekuwa na kampeni ya Serikali (Mkoani Singida 1973) iliyokuwa na lengo la kukomesha tohara ya wanawake iliyotokana na uvumi wa ugonjwa wa lawalawa.

Juhudi za mashirika ya dini zimesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza tohara kwa wanawake. Hali kadhalika, msimamo wa washiriki 275 kati ya 423 katika utafiti uliofanyika (1989), ni kwamba mila hiyo ni mbaya na inastahili kupigwa vita katika taifa zima.

Sura inayofuata, itachunguza kwa undani zaidi aina za kutahiri wanawake. Uchunguzi huu utatupa upeo zaidi juu ya hatari na ubaya wa kutahiri wanawake.

## Sura ya Pili

# AINA MBALIMBALI ZA KUTAHIRI WANAWAKE

Katika sura ya kwanza tumeelezea kuwa shughuli ya kutahiri wanawake huambatana na mila mbalimbali, mbali na kitendo chenyewe.

Katika baadhi ya makabila ya Kiafrika, msimu wa kutahiri, jamii huandaa ngoma, zawadi, vyakula na vinywaji mbalimbali kwa ajili ya sherehe zinazoambatana na mila hii ya kutahiri. Hapa nchini, baadhi ya makabila hufanya matambiko maalum na kutoa kafara ambayo inaweza kuwa mbuzi au kondoo.

Jamii nyingi za kiafrika, hata hapa Tanzania, watu wengi hutahiriwa kwa pamoja. Watahiriwa huwa wana umri wa miaka kati ya mitano hadi kumi. Lakini sehemu zingine kwa mfano Uchagani, wanawake hutahiriwa wakati wa matayarisho ya ndoa.

Pia utafiti uliofanyika hapa nchini (1989) umeonyesha kwamba wanawake wanaoolewa kutoka nje ya utamaduni huu wa kutahiri, au waliokataa walipokuwa na umri mdogo hulazimishwa kuingia katika utamaduni huo kwa njia mbalimbali kwa mfano, wanaweza kutahiriwa wakati wa kujifungua.

Shughuli hii hufanyika katika sehemu maalum kwa mfano nyumbani kwa mganga, katika shamba la migomba, misituni, mbugani, kando kando ya mto, au wakati mwingine hata katika zizi la ng'ombe. Mazingira haya ni machafu na yanaweza yakawa na viini vya magonjwa. Hivyo, mara nyingi vidonda hutunga usaha.

Mtu anayetahiri huitwa ngariba. Ngariba mara nyingi huwa mwanamke mzee ambaye ni maarufu kwa kazi hiyo, au mkunga wa jadi au mganga wa kienyeji.

Wakati wa kutahiri, ngariba hutumia vifaa maalum na hata katika jamii nyingine kwa kutumia kucha ndefu. Ngariba daima humuweka mtahiriwa katika hali ya maumivu makali.

Hata hivyo, mhusika hatakiwi kujichezesha chezesha hata kama maumivu ni makali kupindukia. Vile vile haruhusiwi kuushika mkono wa ngariba au kumzuia kwa namna yoyote. Inaaminika kuwa, iwapo atafanya hivyo atakuwa amevunja miiko. Ili asiweze kufanya hivyo mtahiriwa hushikwa na watu wenye nguvu na hivyo kuwezesha kitendo cha kutahiriwa kwake kuendelea. Kitendo hiki kinahusu kukata viungo mbalimbali vya sehemu za siri za mwanamke.

Ili tuweze kuelewa vizuri aina mbalimbali za kutahiri hatuna budi kuelezea maumbile ya sehemu za siri za mwanamke. Viungo vinavyoonekana ukiangalia sehemu za siri za kike ni kisimi, ngozi inayofunika kisimi ambayo hufanana na ngozi inayofunika kiungo cha kiume (govi), tundu la kutolea haja ndogo, na njia ya uzazi ambayo imezingirwa na mashavu mawili kila upande (shavu dogo la ndani, na kubwa la nje).

Wakati wa kutahiri mwanamke, kimojawapo au zaidi, ya viungo vilivyotajwa hapo juu huondolewa. Ieleweke kwamba hakuna uwezekano wa kiungo kilichokatwa kuota tena.

Ziko aina kuu nne za kutahiri wanawake, kutegemea na kiungo na kiasi gani cha kiungo hicho kimeondolewa.

## 1. Kuondoa Ngozi Inayofunika Kisimi

Ngozi inayofunika kisimi huondolewa kama vile mwanamume anavyotahiriwa kwa kuondoa govi. Katika taifa la Waarabu, aina hii ya kutahiri huitwa suna ambayo maana yake ni *jambo lililo zuri kufanya, lakini siyo la lazima.* Kinadharia, aina hii ya kutahiri ndiyo nafuu kuliko zingine, kwa sababu sehemu inayoondolewa ni ndogo kuliko sehemu zinazoondolewa katika aina zingine za kutahiri.

Hata hivyo maumbile ya asili ya sehemu hiyo huharibika. Jambo la msingi ni kwamba upungufu katika viungo vya asili vya kike, hutokea.

## 2. Kukata sehemu ya Kisimi au Kisimi Chote

Ukataji huu huondoa sehemu tu ya kisimi au kisimi chote, na mara nyingine pamoja na sehemu ya shavu dogo la

sehemu za siri za kike. Katika mila za Kiarabu, kutahiri kwa aina hii huitwa **khefa,** ambayo maana yake ni *kupunguza*. Huu ni uharibifu mkubwa zaidi wa sehemu za siri za kike kuliko ule wa kwanza ulioelezewa hapo awali.

### 3. Kutahiri Kifarao

Viungo viondolewavyo ni ngozi inayofunika kisimi, kisimi chenyewe na mashavu yote ya ndani na nje ya sehemu za siri. Baada ya kuondoa viungo hivi, njia ya kike inayobakia hushonwa pamoja kwa nyuzi za aina mbalimbali au hata nywele kwa kutumia sindano au miiba na kubakiza kijitundu kidogo tu ambamo kijiti, mithili ya ujiti wa kiberiti, hutiwa ndani yake ili kuzuia tundu hilo lisizibe kabisa. Tundu hili huachwa kwa ajili ya kutolea haja ndogo na damu za hedhi. Baada ya kushonwa, miguu ya msichana aliyetahiriwa hufungwa pamoja kwa muda ili kidonda kipone. Uharibifu wote huu eti ni kwa ajili ya kumridhisha mwanamume.

Hii ni aina ya kutahiri ambayo huondoa viungo vingi sana vya sehemu za siri, hivyo basi huambatana na madhara makubwa zaidi.

Aina hii hutumika zaidi katika nchi za Somalia, Sudani na Misri kaskazini mwa Afrika. Katika Tanzania aina hizi tatu ndizo zinazotumika kutahiri wanawake katika makabila mengi, ila tu hawashoni.

### 4. Kupasua Njia ya Uzazi

Aina hii ya kutahiri hufanyika kwa kupasua njia za siri kwa vidole, au kifaa chenye ncha kali na kuingiza chombo maalum ili kupanua njia za uzazi. Hivyo utando wa bikira pia hutobolewa wakati wa kukata njia ya uzazi. Kitendo hiki huambatana na kutokwa na damu kwa wingi na kusababisha kidonda kinapopona kuacha kovu baya sana. Aina hii ya kutahiri imeenea sana katika jamii ya Aborijini, nchini Australia. Hata hivyo, njia hii haitumiki sana siku hizi kwa ajili ya madhara yake makubwa.

Jambo la kusikitisha ni kwamba sababu zinazotolewa za kutahiri wanawake siyo za msingi. Kwa mfano jamii nyingi za

Tanzania, utamaduni wa kutahiri wanawake umejengwa katika imani potofu ambazo humfanya yule anayetahiriwa kukabili kitendo hicho kama kitendo cha ujasiri; humfanya yule anayetahiri (ngariba) kupewa hadhi kubwa na jamii yake na hivyo kuichukulia kazi yake kwa mtizamo huu. Isitoshe, aina zote nne hizo zilizotajwa hapo juu zina madhara makubwa sana kiafya, kisaikolojia na kijinsia, kama itakavyoelezwa katika sura inayofuata.

## Sura ya Tatu

# MADHARA YA KUTAHIRI WANAWAKE

Tohara ya wanawake inatofautiana sana na tohara ya wanaume katika misingi ya afya. Kutahiri wanaume kuna faida za kiafya na kisaikolojia; ambapo kutahiri wanawake kunaharibu kabisa maumbile ya sehemu za siri. Kadhalika kunasababisha madhara yanayohatarisha maisha yao kiafya, na wakati wa uzazi kwa njia mbalimbali.

Madhara ya kutahiri wanawake ni mengi na yanajitokeza katika aina zote za kutahiri zilizoelezwa katika sura ya pili. Kwa kawaida shughuli za kutahiri zinafanywa na watu ambao hawana ujuzi wa kitaalam wa maumbile ya sehemu za siri za mwanamke. Matokeo yake ni kuwa wakati mwingine sehemu zisizokusudiwa zinakatwa na kusababisha madhara yanayojitokeza mara tu baada ya kutahiri au baadaye. Isitoshe hufanyika katika mazingira machafu ikiwa ni pamoja na matumizi ya vyombo visivyokuwa safi na salama. Hali hii inaathiri afya ya mhusika katika maisha yake kama ifuatavyo.

### 1. Madhara Yanayojitokeza Mara tu Baada ya Kutahiriwa au Siku Chache Baadaye

#### *(a) Kutokwa na Damu Nyingi*

Hili ni dhara kubwa ambalo linatokana na kukatwa kwa mishipa ya damu katika sehemu za siri za mwanamke. Kukatika kwa mishipa husababisha damu nyingi ya mtahiriwa kutoka kwa wingi na damu kupungua mwilini. Mara nyingine hali hii husababisha vifo kwa watahiriwa, kwa kuwa siyo rahisi kupata msaada wa kuongezewa damu. Kwa mfano, vifo vingi vilivyotokea huko Singida mwaka 1973 wakati wa lawalawa vilitokana na kutokwa kwa damu nyingi kwa watahiriwa. Katika tukio hilo, watoto wa kike waliotahiriwa ndio waliofariki kwa wingi. Pia katika utafiti uliofanyika hapa nchini, wahusika wengi waliulizwa maswali kuhusu madhara ya kutahiri wanawake, walithibitisha

kuwa kutokwa damu nyingi ni dhara mojawapo linalotishia maisha ya watahiriwa.

Kumbukumbu zilizopatikana katika vituo vya afya vilivyoko katika mikoa ambayo wanawake hutahiriwa, zinaonyesha takwimu za wasichana waliotahiriwa kufikishwa vituoni wakiwa katika hali mbaya, baada ya kutokwa na damu nyingi. Mara nyingi wengi huzimia, na huhitaji kuongezwa damu. Kwa vile vituo vyetu vya afya vijijini havina benki ya damu baadhi ya watahiriwa hupoteza maisha.

### *(b) Maumivu Makali*

Wakati mwingine wahusika huzirai kutokana na maumivu makali kwani kitendo hiki hufanyika bila dawa ya ganzi. Si rahisi kwa watahiriwa kusahau uchungu na maumivu waliyoyapata. Mara nyingi kumbukumbu hii husababisha matatizo ya kisaikolojia katika maisha yao.

### *(c) Kuvimba Sehemu za Siri, na Kushindwa Kukojoa*

Hali hii inatokana na majeraha katika sehemu za kutolea mkojo, na kibofu cha mkojo. Ikiwa anayetahiriwa atashindwa kutulia, na akajitikisa tikisa kwa sababu ya maumivu, anaweza kupata jeraha katika sehemu hizo.

Utafiti uliofanyika hapa nchini, (1988 na 1989) ulionyesha kwamba wanawake waliotahiriwa walipata maumivu makali sana wakati wa kukojoa. Pia walisema kuwa walipata maumivu makali hata kushindwa kukojoa. Mara nyingi imebidi watafute msaada hospitalini.

### *(d) Uambukizo (Kutunga Usaha)*

Uambukizo hutokana na matumizi ya vifaa vichafu na mazingira machafu wakati wa kutahiri. Hali hii ya uambukizo hutokana na vijidudu kushambulia kidonda na hivyo huzidisha uvimbe wa jeraha. Pengine sumu husambaa mwilini na inaweza kusababisha kifo. Vijidudu vibaya sana ni vile viletavyo pepopunda. Mara nyingi matokeo ya pepopunda ni kifo. Vile vile UKIMWI, (AIDS), ugonjwa ambao hauna tiba, unaweza kuambukizwa kwa kutumia vifaa vichafu vya kutahiria.

## 2. Madhara Katika Maisha ya Baadaye

Ikiwa mtahiriwa atanusurika madhara yaliyotajwa hapo juu, bado madhara mengine yaweza kumwandama baadaye. Madhara hayo ni kama kuota kinundu kwenye kovu (Keloid), matatizo wakati wa kujifungua, ugumba, na matatizo ya kijinsia na ya kisaikolojia.

### *(a) Kuota Kinundu Kwenye Kovu, (Keloid)*

Hii inaweza kutokea kwa baadhi ya watu; kwa mfano baadhi ya watu wakitoga masikio huota vinundu. Kadhalika sehemu za siri zikikatwa, kama ifanywavyo wakati wa kutahiriwa, kunaweza kuota kinundu na kuharibu sura nzuri ya sehemu za siri za mwanamke. Pia inaathiri kitendo cha kujamiiana kwa sababu mwanamke anapata maumivu badala ya starehe.

### *(b) Matatizo Wakati wa Kujifungua*

Matatizo haya huwakabili hasa wanawake waliofanyiwa ile aina ya tatu ya tohara **Kifarao**, iliyoelezwa hapo mwanzo. Kwa sababu wanashonwa njia ya uzazi inakuwa nyembamba na huchelewesha mtoto kuzaliwa. Mara nyingine mtoto anaweza kufia tumboni. Aidha kovu huchanika vibaya na kusababisha mama kupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua. Utafiti uliofanyika mikoa ya Singida na Dodoma (1989), unaonyesha kuwa karibu watahiriwa wote waliohojiwa walidhihirisha kuwa walipata matatizo ya kuchanika na kupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua.

### *(c) Ugumba*

Ugumba unaweza kutokea ikiwa mtahiriwa ameshambuliwa na vijidudu vya magonjwa, na vikasambaa hadi kwenye mfuko wa kizazi na njia zake. Vijidudu hivi husababisha kuziba kwa mirija ya kizazi na baadaye mama hushindwa kutunga mimba.

## *(d) Matatizo ya Kijinsia na Kisaikolojia*

Imedhihirika katika utafiti uliofanywa sehemu mbalimbali barani Afrika, kuwa kitendo cha kumtahiri mwanamke kinaathiri sana maisha yake ya baadaye. Kwa mfano, hamu yake ya kujamiana hupungua sana; na maumivu makali hutokea wakati wa kufanya kitendo hiki.

Kisaikolojia uchunguzi umeonyesha ya kuwa wanawake hawa hujisikia pungufu na wanakosa raha kwa vile wametahiriwa. Pia matatizo katika unyumba yanatokea, kama vile kutengana na kuoa wake wengi. Katika sehemu zingine za Afrika, utafiti umeonyesha kuwa matatizo yanaweza kusababisha tabia ya ulawiti ambayo huleta madhara makubwa. Matokeo ya matatizo hayo yote wakati mwingine ni kuvunjika kwa unyumba.

Mila na desturi za jamii zinazotahiri wanawake zina lengo la kumtawala, na kumdhalilisha mwanamke. Sehemu nyingi hapa Tanzania wanawake bado hawana sauti katika jamii. Ndiyo maana siyo rahisi kwa wanawake walioko kwenye jamii yenye mila hiyo kukataa bayana kitendo cha kutahiriwa.

Kwa kuzingatia athari za kutahiri wanawake, ni muhimu jamii nzima ishiriki kikamilifu katika kukabili tatizo hili, na kutokomeza mila hii na zingine zilizo potofu.

# Sura ya Nne

## MBINU NA MIKAKATI YA KUKABILI NA KUTOKOMEZA MILA ZA KUTAHIRI WANAWAKE

Sura zilizotangulia zimeonyesha waziwazi athari zitokanazo na kutahiri wanawake; hivyo kutahiri wanawake kukomeshwe. Tohara ya wanawake kama tulivyoona inaambatana na matatizo mengi ya afya, saikolojia na kadhalika. Jambo hili linapigwa vita na jamii nyingi duniani pote.

Ingawa utafiti umefanyika sehemu chache tu, umeonyesha kuwa kutahiri wanawake kuna madhara makubwa. Hata hivyo bado nchi nyingi za Afrika, ikiwemo Tanzania, zinaendelea kutahiri wanawake. Vilevile, ni nchi chache tu zilizochukua hatua za kukabili tatizo hili kama vile Somalia na Sudani.

Jambo la kutahiri wanawake halijapewa uzito unaostahili kama tatizo la kiafya na kijamii hapa Tanzania na mahali pengine duniani. Haujafanyika utafiti wa kutosha juu ya madhara ya kutahiri wanawake. Zipo kumbukumbu chache kuhusu matatizo, athari, na maafa au vifo vinavyosababishwa na kutahiri wanawake. Kumbukumbu hizo hazipatikani katika jamii nyingi kwa sababu kutahiri wanawake mara nyingi hufanywa kwa siri.

Jamii zinazotahiri wanawake zina imani potofu kuhusu mila na desturi hii. Mila ya kutahiri wanawake inaambatana na usiri pamoja na vitisho vingi kwa asiyetahiriwa na aliyetahiriwa. Vyombo vinavyohusika na elimu ya jamii kwa mfano Chama na jumuiya zake, vyombo vya habari na kadhalika, havijaweka umuhimu katika kukabili tatizo hili. Wataalam wa afya hawajafanya jitihada kubwa ya kupiga vita kitendo cha kutahiri wanawake. Hata jamii yenyewe bado haijafanya jitihada za kutosha katika kulikabili tatizo hili.

Kama ilivyoelezwa katika sura zilizotangulia, Tanzania ina zaidi ya mikoa saba ambayo inakabiliwa na tatizo la kutahiri wanawake. Hivyo, tatizo hili linawahusu watu wengi. Ni muhimu kuhamasisha na kuuelimisha umma juu ya madhara ya kiafya na ubaya wa utamaduni huu.

Njia zifuatazo zinafaa kutumiwa katika kukabili tatizo hili.

## 1. Elimu kwa Umma

Jamii ndiyo inayoendeleza mila hii potofu ya kutahiri wanawake. Kwa hiyo jamii ina jukumu la kukomesha utamaduni huu. Vyombo na Taasisi mbalimbali vinavyohusika na elimu havina budi kuelimisha jamii juu ya madhara ya kutahiri wanawake.

Wizara ya Elimu ni chombo muhimu katika kutokomeza utamaduni huu. Wizara ya Elimu ina mipango ya elimu ya msingi kwa wote, kisomo cha manufaa na elimu kwa jamii ambayo inaendeshwa nchini pote. Hivyo basi, somo la Madhara na Hatari za Kutahiri Wanawake lingeingizwa katika mihtasari iliyotajwa hapo juu. Wanafunzi katika madarasa ya kisomo, shule za misingi na sekondari hawana budi kufundishwa kikamilifu juu ya ubaya wa madhara ya kutahiri wanawake. Elimu hii itawezesha wanafunzi mashuleni kutambua ubaya wa kutahiri wanawake na kuukataa.

Vyuo vya maendeleo ya wananchi pia ni nafasi mojawapo nzuri ya kuwapatia maelezo wanaume na wanawake juu ya athari ya kutahiri wanawake. Vyuo hivi hupokea wanafunzi kutoka vijijini. Baadhi ya wanafunzi ni viongozi au watu maarufu katika jamii zao. Kwa hiyo muhtasari wa vyuo hivi utawawezesha wanafunzi kuelewa madhara ya tohara ya wanawake na kupiga vita mila hii.

Ili kufanikisha suala zima la kutahiri wanawake, hakuna budi kushirikisha sekta mbalimbali; kwani kukomesha mila ya kutahiri wanawake ni suala la wote.

Idara ya sheria ishiriki kikamilifu katika kutatua tatizo hili. Zitungwe sheria zinazolinda haki za wanawake, pamoja na kutokomeza mila hii ya kutahiri wanawake. Ili kufanikisha utekelezaji wa sheria hizi, jamii itoe taarifa kwa Chama na Serikali kuhusu wanaoendelea kutahiri wanawake. Hii itaviwezesha vyombo hivyo kuchukua hatua zinazofaa.

Wizara ya Afya iimarishe mafunzo yake ya Elimu ya Afya kwa Umma. Aidha mihtasari ya mafunzo ya waganga wa jadi ieleze wazi wazi madhara ya kutahiri wanawake. Wizara ya Afya ifanye utafiti zaidi juu ya matatizo ya kiafya yanayotokana na kutahiri wanawake, ili iweze kutoa ushauri kwa umma.

Vile vile, mafunzo yanayoendeshwa hapa nchini kama 'Family Life Education' pamoja na uzazi wa mpango na uhai na ukuzi wa mtoto, yaambatane na programu ya kupiga vita ya kutahiri wanawake.

## 2. Mbinu

Elimu kwa jamii juu ya tatizo la kutahiri wanawake iandaliwe na kutolewa kwa kutumia mbinu zifuatazo:

### *a. Vipindi Mbalimbali vya Radio*

Vipindi vya radio vieleze bayana matatizo na hatari za tohara ya wanawake. Vikundi vya akina mama, wanaume, vijana na wazee wajadili matatizo ya kiafya, kisaikolojia, kijamii na kiuchumi yanayoambatana na kutahiri wanawake.

Mashehe, wachungaji na mapadri waanzishe mjadala wa waumini wao juu ya ubaya wa mila hii potofu ya kutahiri ili waweze kutambua ubaya huo na kukubali kuacha kabisa kutahiri watoto wao. Waalimu katika mashule na madarasa ya kisomo, pia waanzishe mijadala ya namna hiyo na kuifuatilia kwa vitendo.

Vikundi vya sanaa, hasa katika ngazi ya kijiji vibuni na kuigiza michezo inayoonyesha madhara na kukataza kutahiri wanawake.

### *b. Magazeti*

Magazeti ya Chama na Serikali, kwa mfano 'Uhuru', 'Mzalendo', 'Mfanyakazi' na 'Daily News' yabuni mfumo wa kuchokoza mawazo kutoka kwa jamii juu ya tatizo la tohara ya wanawake. Mawazo haya yatatoa mchango mkubwa katika kulikabili tatizo hili.

Magazeti ya kanda na ya jumuiya za dini kama 'Kiongozi', 'Njoo Uone' na 'Muislam' yaongelee masuala yanayohusu jamii na tohara ya wanawake. Magazeti yatoe kipaumbele katika kutoa nafasi kwa jamii, hasa wanawake, ya kuchambua suala zima la tohara ya wanawake.

Taarifa za matatizo yote ya kiafya, kijamii na kisaikolojia, kutoka kwa wahusika katika tohara ya wanawake zipewe uzito mkubwa zaidi. Magazeti yenye habari hizi yasambazwe

kote nchini. Vyombo mbalimbali vinavyohusika na usambazaji wa magazeti haya viimarishe na kubuni mbinu za kusambaza magazeti ili yawafikie wananchi.

### *c. Semina, Kongamano na Mihadhara*

Semina, kongamano na mihadhara kwa viongozi wa Chama na Jumuiya zake, Serikali, mashirika mbalimbali mikoani na wilayani na madhehebu ya dini, vitumike kama nyenzo za kuwahamasisha kuanzisha mijadala na kubuni mbinu na mikakati ya kukabili mila hii potofu. Nyenzo hizi pia zinawezesha kufuatilia na kutathmini maendeleo ya hatua zinazochukuliwa kukabili tatizo la kutahiri wanawake katika maeneo yao. Vitabu, mabango, na vitini vitolewe kama vielelezo vya kuimarisha kampeni ya kufuta mila ya kutahiri wanawake.

Utaratibu huu wa kutoa mafunzo juu ya tohara ya wanawake utatumika pia katika kuwahamasisha, kuwaelimisha na kuanzisha mijadala ya kubuni mbinu na mikakati ya kutokomezwa mila hii miongoni mwa wananchi katika ngazi mbalimbali na vikundi. Kuna umuhimu wa kuzingatia mahitaji na matakwa ya wanawake katika mafunzo haya.

### *d. Kupeana Habari Kwa Mbinu za Jadi*

Hapa Tanzania, kutahiri wanawake mara nyingi kunaambatana na tambiko na sherehe za ngoma na nyimbo. Shughuli hii ya kutahiri ni ya msimu. Ngoma na nyimbo hizo hutukuza mila hii ya kutahiri wanawake, ili kuwavutia hasa vijana wa kike ambao hawajatahiriwa, ngariba, na wazazi katika jamii hizo waiendeleze mila hii.

Ngoma na nyimbo zinaweza zikatumika katika kubadili mtazamo wa jamii kuhusu utamaduni huu. Kwa mfano wanafunzi mashuleni, vijana na vikundi vya kisomo waimbe nyimbo na kucheza ngoma zinazoeleza ubaya na kupinga kitendo cha kuendelea kutahiri wanawake. Wanawake, wanaume, vikundi vya sanaa pia washiriki kikamilifu. Ujumbe uliomo katika ngoma na nyimbo hizo huwawezesha wazazi, watahiri, watahiriwa na viongozi katika mikutano ya hadhara, kuona uzito wa tatizo hili na walitafutie ufumbuzi.

## 3. Jukumu la Jamii

Jukumu la kuondoa mila ya kutahiri wanawake ni la kila mtu katika jamii. Kiutekelezaji, Chama na Jumuiya zake, Serikali Kuu na za Mitaa na madhehebu ya dini na mashirika yanayojitegemea (NGO), vina jukumu kubwa katika kukabili tatizo hili.

### *Chama na Jumuiya Zake*

Chama hapa nchini kina uwezo mkubwa wa kufikisha ujumbe juu ya madhara ya kutahiri wanawake kwa wananchi; kwa sababu Chama kipo kila mahali. Chama hakina budi kuchukua jukumu la kushirikisha viongozi wa ngazi zote toka taifa hadi kijiji na wananchi, na kufuatilia juhudi zote zinazochukuliwa kukabili mila hiyo potofu.

Jumuiya za Chama nazo, zinayo nafasi nzuri ya kuelimisha umma juu ya madhara ya kutahiri wanawake. Wanachama wa jumuiya hizi wanahusika sana na tatizo hilo kwa njia moja au nyingine, mathalan kutahiri, kutahiriwa au kutoa uamuzi juu ya suala hili.

### *Jumuiya ya Wazazi*

Jumuia ya Wazazi haina budi kuelimisha wazazi na jamii kwa ujumla juu ya madhara ya kutahiri wanawake. Wazazi ndio wenye maamuzi, na ndio wanaotahiri watoto wa kike. Kwa hiyo wazazi wana uwezo na wajibu wa kutokomeza mila hii. Jumuiya ya wazazi ishirikiane na wazazi kukomesha mila hii.

### *Jumuiya ya Wanawake*

Kwa vile Jumuiya ya Wanawake ipo karibu sana na wanawake katika jamii, lazima ichukue jukumu la kuwahamasisha, kuwaelimisha wanawake na jamii juu ya tatizo hili. Hii itawapa mwamko na msimamo wa kuliangalia tatizo hili kwa mapana yake.

Mwenyekiti wa CCM, Mwalimu J.K. Nyerere, (Mei 1988), akifunga semina ya Halmashauri Kuu ya Taifa ambayo ilizungumzia masuala ya wanawake, alisema kuwa, haoni ni kwa

sababu gani mila ya kutahiri wanawake isipigwe marufuku. Kwa hiyo msimamo huu ufuatiliwe. Wakati umefika wa kutunga sheria ya kuondoa mila hii na nyinginezo zinazodhalilisha utu wa mwanamke.

*Jumuiya ya Vijana*

Jumuiya ya Vijana ina uwezo mkubwa katika kuelimisha watu juu ya tatizo hili. Vijana ndio wanaotahiriwa na ndio wazazi wa baadae. Ikiwa vijana wataelewa ukubwa na uzito wa tatizo hili wataweza kutoa mchango mkubwa kwa kushirikiana na Chama na Serikali katika kutokomeza utamaduni huu. Mathalani vijana wawe mstari wa mbele katika kutoa mafunzo na kuunga mkono jitihada zote zinazopiga vita.

## 4. Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma

Suala la kutahiri linahusu haki na uhuru wa mwanamke, utamaduni, na maendeleo ya nchi. Hivyo Serikali kuu, Serikali za Mitaa na mashirika ya Umma hayana budi kulipa tatizo hilo uzito unaostahili. Wanawake kwa wanaume waelimishwe na juhudi zifanywe kusimamia sheria zinazokataza kutahiri wanawake pamoja na mtazamo wa kijinsia kuhusu utamaduni wa kutahiri wanawake. Elimu hii inawahusu watu wote; wakubwa kwa wadogo, ili kuiondoa kabisa imani hii potofu. Pia ijengwe misingi ya mawazo bora kwa vijana kwa kuingiza somo hili katika muhtasari wa shule, vyuo, na shughuli zote za jamii.

## 5. Madhehebu ya Dini Mbalimbali

Vita vya kukabili tatizo la kutahiri wanawake lazima vifanywe na jumuiya zote. Waumini wengi wana imani kubwa na viongozi wao wa dini. Viongozi wa dini wamefanikisha kampeni nyingi hapa nchini, kwa mfano, kampeni ya chanjo. Ni wajibu wa madhehebu mbalimbali kuwa mstari wa mbele katika kukemea na kutokomeza mila ya kutahiri wanawake.

### 6. Mashirika Yanayojitegemea (NGO)

Mashirika mengi ya kujitegemea kama vile UMATI, CHEWATA, YMCA, YWCA, CCT, TAMWA na Msalaba Mwekundu yanatoa huduma zilizo karibu na wananchi. Kwa hiyo wanalo jukumu kubwa la kuunga mkono juhudi za wananchi na taifa dhidi ya mila hii ya kutahiri wanawake.

VITA DHIDI YA KUTAHIRI WANAWAKE

| | | |
|---|---|---|
| | CHAMA NA JUMUIYA ZAKE | MADHEHEBU YA DINI |
| MASHIRIKA YANAYOJITEGEMEA (NGO) | TATIZO LA KUTAHIRI WANAWAKE | SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YAKE |
| SERIKALI ZA MITAA | SERIKALI ZA KIJIJI | |

Mafanikio katika vita dhidi ya kutahiri wanawake ni jukumu la jamii na vyombo vyake. Hivyo jumuiya zote hizi zishirikiane kuondoa tatizo la kutahiri wanawake.